HALMASHAURI YA MANISPAA YA TABORA

SHULE YA SEKONDARI KANYENYE
S.L.P. 1314, **TABORA**.

Kumb. Na. S.3115/J.10/VOL.I/10 Tarehe: 15/12/2020

Jina la Mwanafunzi: ……

S.L.P. ……

……

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KANYENYE

1.0. **Utangulizi**:

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza mwaka 2021 katika Shule hii. Shule ya Sekondari Kanyenye ipo katika eneo la Malolo barabara iendayo Wilaya ya Urambo, umbali wa Kilometa 3 kutokea Stendi Kuu ya Mabasi.

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 11/01/2021 na unatakiwa kuripoti siku hiyo. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 18/01/2021 ndani ya siku saba.

2.0. Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1. Sare za Shule

(a) Wavulana

(i) Shati nyeupe (tetron) ya mikono mifupi isiwe na maua. Hii ichomekwe ndani ya suruali wakati wa kuvaliwa;

(ii) Suruali ya rangi ya kijivu iliyoiva (angalia kitambaa) isibane mwili

(iii) Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunika miguu, view vyenye visigino na sori fupi;

(iv) Soksi nyeupe au kahawia

(v) Tai inayofanana na kitambaa cha suruali;

(vi) Sweta lifanane na rangi ya suruali

(b) **Wasichana**

(i) Blauzi/Shati nyeupe (tetron) ya mikono mifupi, isibane mwili kuonesha nguo za ndani na isiwe na maua. Hii ichomekwe ndani ya Sketi wakati wa kuvaliwa;

(ii) Sketi ya rangi ya kijivu iliyoiva (angalia kitambaa) iwe ndefu chini ya magoti, na isiwe na marinda mapana;

(iii) Viatu vya ngozi vyeuzi vya kufunika miguu vyenye kisigino na sori fupi;

(iv) Soksi nyeupe ndefu isiwe na mchanganyiko wa rangi;

(v) Tai inayofanana na kitambaa cha sketi;

(vi) Sweta lifanane na rangi ya sketi;

(vii) Rangi ya Hijab ifanane na sare za Shule (angalia mshono);

(c) Sare za Michezo

Sare ya michezo kwa Wavulana na Wasichana ni TShirt na Bukta zote zenye rangi ya Bluu-Nyeusi (Dark blue) pamnoja na raba ya aina yoyote.

2.2. Daftari kubwa zisizo pungua 10, Kalamu za Wino, Penseli na Mkebe wa Hesabu

3.0. Sheria na Kanuni Muhimu za Shule hii

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

(a) Heshima kwa Viongozi, Wazazi, Wafanyakazi wote, Wanafunzi wengine na Jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;

(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulinga na ratiba ya shule ni lazima;

(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation);

(d) Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa;

(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

(g) Kuvaa sare ya shule wakati wowote unapotakiwa;

(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na;

(i) Kutunza mali za umma.

3.2. Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule

(a) Wizi

(b) Uashereati na Ushoga

(c) Ubakaji

(d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, Cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika

(e) Kupigana au kupiga

(f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma

(g) Kudharau Bendera ya Taifa

(h) Kuwa mjamzito/kupata mimba

(i) Kuoa au kuolewa

(j) Kutoa mimba

(k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu

(l) Kukataa adhabu kwa makusudi

(m) Kuwa na simu ya mkononi

4.0. Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi

(a) Medical Examination form, ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakapo ripoti shuleni

(b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai

(c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule

5.0. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatakeleza kikamilifu

KARIBU SANA

P. KAPUFI
MKUU WA SHULE

FOMU YA MAKUBALIANO

1. SEHEMU YA MWANAFUNZI:

Mimi _____ nimeyasoma na kuyaelewa maagizo pamoja na mwongozo wa mambo ya kuzingatia shuleni. Nanaipokea nafasi hii niliyopewa na Taifa kuwa mwanafunzi wa Kutwa Shule ya Sekondari Kanyenye, naahidi kuzitekeleza Sheria na Kanuni za Shule na kuzingatia masomo yangu kama inavyotakiwa kinyume chake nichukuliwe hatua zinazostahili.

Sahihi: _____ Tarehe: _____

2. SEHEMU YA MZAZI/MLEZI

Mimi _____ Mzazi/Mlezi wa _____ nimeyasoma na kuyajadiliana na mwanangu maagizo haya. Nimeikubali nafasi hii aliyopewa mtoto wangu na nitamtimizia mahitaji yake yote kama mwanafunzi wa kutwa. Aidha nitahakikisha muda wote anazingatia sheria na taratibu za shule.

Sahihi: _____ Tarehe: _____

3. **MWISHO**:

Nitumaini letu kwamba mwanao atafurahia na kujivunia shule yake mpya. Hivyo tunamkaribisha na kumtakia mafanikio mema. Kwa kukubali nafasi hii tujazie fomu hii ili mwanao aje nayo siku ya kuripoti.

_____

MKUU WA SHULE

MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY

KANYENYE SECONDARY SCHOOL,
P.O. Box 1314,
TABORA.

Date: _____

FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

This Form must be completed by a Government Medical Officer

Student's full name: _____

Presents Age: _____

Blood test: _____

Stool Examination: _____

T.B. Test: _____

Asthma: _____

Eye Disorder: _____

Nose disorder: _____

Ear disorder _____

Skin disease: _____

Anemia: _____

Chest: _____

Operations: _____

Serious Accidents: _____

Any other infection disease: _____

Pregnancy: _____

ADDITIONAL INFORMATION E.g. Physical defects or impairment, chronic or family diseases etc _____

_____

I certify that I have personally examined Mr./Miss _____ and found him/her fit/unfit to pursue studies.

Signature: _____
Designation: _____
(Official rubber stamp)